

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO



TANGAZO KWA WADAIWA SUGU WA MADENI YA MFUKO WA CHAKULA WA PAMOJA KATI YA TANZANIA NA JAPAN - FAF

Kati ya mwaka 1978 hadi 2013, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipokea msaada wa chakula (mchele), mbolea, madawa (viatilifu) na zana za kilimo chini ya mpango wa KR-I (Mchele) na KR-II (Pembejeo za kilimo) kutoka Serikali ya Japan.

Mchele na mbolea vilipokelewa kati ya mwaka 1978 hadi 1999, na kuuzwa kwa mkopo kwa makampuni ya umma na binafsi ili wauze kwa bei nafuu kwa wananchi na baadaye makampuni hayo yarejeshe mkopo katika Mfuko wa FAF ndani ya mwaka mmoja. Hata hivyo baadhi ya makampuni yaliyofaidika hayakukamilisha marejesho, hivyo kusababisha madeni ya muda mrefu.

Ili kuhakikisha wadaiwa wote wanalipa mikopo yao, Serikali imeunda Kikosi Kazi ambacho kinajukumu la kufuatilia na kukusanya madeni toka kwa wadaiwa wote ili fedha hizo ziweze kutumika kwa miradi ya maendeleo. Serikali inawataka wadaiwa wote kulipa madeni hayo ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya kutolewa kwa tangazo hili. Kwa wote ambao hawatarejesha mikopo hiyo katika kipindi cha siku 30, majina yao yatatangazwa katika vyombo vya habari na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Kikosi Kazi, Wizara ya Fedha na Mipango, Dar es Salaam, chumba Na. 352, Simu Na. +255 739 40 30 25.

**KATIBU MKUU
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

